

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE

Shule ya Sekondari Munanila

S.L.P 178

BUHIGWE

Mzazi wa: _____

10th December, 2020

SHULE YA MSINGI _____

BUHIGWE

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUNANILA
KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

1.0: UTANGULIZI

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa, Mtoto wako amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Munanila mwaka 2021. ***Hongera sana!!*** Ni matumaini yangu fursa hii ataitumia ipasavyo ili kutimiza ndoto zake na kuwa mfano wa kuigwa katika jamii na Taifa kwa jumla.

Muhula wa masomo utaanza siku ya **Jumatatu** tarehe **11.01.2021** saa **1:00 Asubuhi**. Mwanafunzi afike shuleni akiwa na mzazi/mlezi kuanzia tarehe 06.01.2021 kwa ajili ya usajili na kuanza masomo ya awali. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe **25.01.2021**. Mwanafunzi asiye fika shuleni bila mzazi/mlezi **hatapokelewa**. Hata hivyo, mwanafunzi aje na **daftari moja tu kubwa** (counter book Q4) pamoja na kalamu na Rula. Tafadhari zingatia agizo hili.

2.0: SARE ZA SHULE

2.1: WAVULANA

- Suruali mbili rangi ya **Dark Blue** (Fika shuleni ili upate rangi au fika kwa fundi yeyote atakuelekeza) zenye marinda 2 na mfuko mmoja nyuma (Modo haziruhusiwi)
- Mashati mawili meupe mikono mifupi
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visigino vifupi pamoja na soksi pea mbili **nyeusi**
- Raba za michezo nyeupe na Soksi za Bluu ndefu
- Suruali **Nyeusi**, Bukta ya Bluu ya michezo pamoja na Flana ya Bluu isiyokuwa na maandishi
- Sweta kwa ajili ya baridi rangi **Damu ya mzee** lenye kola ya **V**
- Begi kwa ajili ya kubebea madaftari.

2.2: WASICHANA

- Sketi mbili rangi **Dark Blue (Linda Box)** kitambaa kizito zenye marinda zinazovuka magoti.
- Mashati mawili meupe mikono mifupi
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visigino vifupi pamoja na soksi **ndefu** pea mbili nyeupe
- Raba za michezo nyeupe
- Sketi moja **Nyeusi** ya michezo pamoja na Flana ya Bluu isiyokuwa na maandishi
- Sweta kwa ajili ya baridi rangi **Damu ya mzee** lenye kola ya **V**
- Waschana wa Kiislamu wavae jubaa ndefu nyeupe inayofunika mwili vizuri, sketi ndefu inayofunika miguu na shati nyeupe mikono mirefu.
- Begi kwa ajili ya kubebea madaftari

3.0: MAHITAJI MENGINE YA JUMLA

- Daftari kubwa 9 (Counter Books 3 Quires), Kalamu, Rula, Penseli na mkebe wa Hesabu
- Dictionary/Kamusi moja kwa ajili ya rejea kwa masomo ya Kiingereza
- CHETI cha kuzaliwa (Nakala) au kiapo cha Mahakamani (Nakala – Affidavit Form)
- Fomu ya vipimo Hospitalini (Medical Examination Form) yenye majibu ya vipimo
- Tai ndogo (neck tie) rangi **dark blue**
- Karatasi nyeupe (Ream moja) tu kwa mwaka
- Truck suit rangi nyeusi

4.0: MUHIMU

Kila mwanafunzi asome kwa makini sheria za shule zilizoambatanishwa na maelekezo haya na atapaswa kuzifuata muda wote awapo shuleni. **KARIBU** sana Shule ya Sekondari Munanila – BUHIGWE!

MALONGO, L.A
MKUU WA SHULE

Nakala;

- Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya Buhigwe
S.L.P 443

BUHIGWE

[Aione kwenye jalada]

- Mwenyekiti wa Bodi wa Shule
Shule ya Sekondari Munanila
S.L.P 178

BUHIGWE

[Kwa taarifa]

- Afisa Elimu Kata
Kata ya Munanila

BUHIGWE

[Kwa taarifa]